

HUDUMA YA KUAGIZA MTANDAONI KWA WIC SASA INAPATIKANA WALMART!

NUNUA MTANDAONI ILI UNUNUE VYAKULA VYA WIC KWA URAHISI

- Chagua wakati wa kupokea au kuchukua ambao unakufaa.
- Tafuta tu bidhaa zinazotimiza masharti ya WIC.

JUA KABLA HUJAINGIA MTANDAONI

- Chagua duka la Walmart popote pale Washington.
- Angalia salio lako la manufaa kwenye programu ya WICShopper au kwenye tovuti ya Walmart.
- Nunua mapema! Uchukuaji, uwasilishaji na ubadilishanaji lazima ufanyike **katika kipindi chako cha sasa cha manufaa**.
- Angalia ili kuona ikiwa uwasilishaji ni chaguo katika eneo lako.
» Tafadhal kumbuka: WIC haigharamii ada za uwasilishaji.

Nunua Mtandaoni Kwa Kutumia Tovuti au Programu ya Walmart

Walmart | Okoa Pesa. Ishi Maisha Bora.


Pakua programu ya Walmart.



Kwa Maswali na Usaidizi Wasiliana na Kituo cha Usaidizi cha Walmart

Msaada - Walmart.com

Simu: 1-800-925-6278





JINSI YA KUANZA

- Nenda kwenye Walmart.com au ufungue programu ya Walmart.
- Bofya "Sign in (Ingia)" au "Create an account (Fungua akaunti)."
- Bofya "Add new payment method (Ongeza njia mpya ya malipo)" au "Add payment card (Ongeza kadi ya malipo)" na uweke nambari yako ya kadi ya WIC na PIN.

JINSI YA KUNUNUA

Kuna njia 2 za kutafuta vyakula vyta WIC.

1. Tumia upau wa utafutaji.

- Weka chakula unachotafuta.
- Tafuta lebo ya "WIC Eligible (Inastahiki WIC)".
- Bonyeza "+Add (+Ongeza)"
- Tafadhali kumbuka: Walmart inaweza kuonyesha bidhaa zaidi ambazo hazistahiki WIC. Angalia lebo ya "WIC Eligible (Inastahiki WIC)" na orodha yako ya manunuzi ili uthibitisha manufaa ya chakula yanayopatikana katika akaunti yako.

2. Nunua manufaa yako ya WIC

- Chagua orodha kunjuzi ya **Services (Huduma)**
- Chagua **Online Ordering (Kuagiza Mtandaoni)**.
- Chagua **WIC** chini ya **Benefits Programs (Mipango ya Manufaa)**.
- **ONGEZA** vyakula vyako vinavyostahiki WIC.

JINSI YA KULIPA

1. Bofya kwenye **Shopping Cart (Kikapu cha Manunuzi)**.
2. Chagua **Pickup (Kuchukua)** au **Delivery (Uwasilishaji)** na uchague siku na saa.
 - » Upatikanaji wa uwasilishaji unategemea anwani.
3. Bofya "**Continue to check out (Endelea ili ulipe)**."
4. Weka **PIN yako ya WIC**.
5. Kagua oda yako na chaguo lako la malipo.
6. Bofya "**Place order (Weka oda)**".
 - » Weka PIN ya WIC tena ili kuidhinisha matumizi ya kadi yako ya WIC.

Orodha yako ya manufaa itasashwa pale oda yako itakapowekwa.

VIDOKEZO:

Una majaribio 4 ya kuweka PIN yako kabla ya akaunti yako kufungwa hadi saa sita usiku.

Walmart inakuhitaji uweke njia ya pili ya malipo ukichagua kuwasilisha au kuwa na bidhaa zozote zisizo za WIC katika oda yako.